



IDARA YA SERIKALI KUU YA LEBA

MKATABA WA UTOAJI HUDUMA KWA WANANCHI

RUWAZA: Wafanyikazi walio na ustadi

LENGO LETU: Kukuza ufanyikazi wenye hadhi, ujuzi wa kikazi na pia ubunifu endelevu wa ajira

MAADILI MSINGI

- Ukuzaji wa kanuni bora za utendakazi nchini.
- Viwango vya hali ya juu vya usalama katika mahali pa kazi.
- Utendakazi wenye tija/mazao.
- Ushirikishwaji sawa wa Wakenya wa asili mbalimbali katika ajira.

VIGEZO VYA HUDUMA ZETU

	HUDUMA	JUKUMU LA MTEJA	MALIPO	MUDA WA KUSHUGHULIK IWA
1.	Kutatua malalamishi ya Kikazi	-Ushirikiano wa wafanyikazi na waajiri -Kufuata sheria za Leba	Hamna	Katika muda wa siku 45

2.	Uchunguzi wa migogoro ya kikazi na kuandaa taratibu za upatanisho.	-Ushirikiano wa vyama vya wafanyikazi na vya waajiri -Kuzingatia sheria za Leba	Hamna	Katika muda wa siku 45
3.	Uthibitisho wa kandarasi za kigeni	Ushirikiano wa watafutao kazi, waajiri na mashirika ya uajiri/mawakala	Dhamana ya shirika husika/ mwajiri/wakala.	Siku mbili
4.	Uchunguzi wa mikataba ya maafikiano kati ya waajiri na waajiriwa (CBAs) kabla ya kusajiliwa na Mahakama ya Wafanyakazi	Hati za mkataba/ nakala 3 za CBA zilizotiwa sahihi.	Hamna	Siku tano
5.	Usajili wa vyama vya wafanyikazi	Kujaza fomu A kikamilifu.	Shilingi 15,000	Katika muda wa Mwezi moja
6.	Ukaguzi wa vitabu vya hesabu/ akaunti vya vyama ya wafanyikazi	Vitabu vya hesabu vilivyoagizwa katika Labour Relations Act, 2007	Hamna	Siku moja
7.	Ukaguzi wa hali ya afya ya wafanyikazi	Kupatikana kwa wafanyikazi ili wakaguliwe	Shilingi 500 pasipo kuhesabu malipo ya vipimo vya ziada.	Siku tano
8.	Kutayarisha hati ya malipo ya kufidia majeraha kazini	Kujulisha Wizara ajali au ugonjwa kwa kujaza stakabadhi 'DOSH Form 1' kikamilifu	Hamna	Siku kumi na nne
9.	Kutekeleza mikakati ya kuboresha uzalishaji katika makampuni	Makubaliano na wamiliki ama wasimamizi wa Kampuni.	Hamna	Miezi sita
10.	Kufanya utafiti juu ya viwango vya uzalishaji katika kampuni	”	Hamna	Mwezi moja
11.	Kutoa habari juu ya hali ya soko la ajira (Labour Market) kwa washika dau	Kufungua mtandao www.labourmarket.go.ke	Hamna	Papo hapo
12.	Kulipia bidhaa kwa wateja wa ndani na nje baada ya kupokea fedha kutoka kwa Hazina ya	Kuwasilisha stakabadhi zilizo idhinishwa	Hamna	Siku tatu

	Kitaifa			
13.	Kutoa majibu kwa barua zilizopokelewa	Kuwasilisha barua	Hamna	Siku tatu
14.	Kutoa majibu kwa wanao uliza kupitia simu	Mteja kupiga simu	Hamna	Mlio wa simu mara zisizozidi tatu

TUMEJITOLEA KWA HUDUMA BORA

Huduma yoyote isiyoambatana na vigezo vya huduma vilivyotajwa hapo juu viripotiwe kwa:

KATIBU MKUU, IDARA YA LEBA

JENGO LA NSSF, BLOCK 'A' GHOROFA YA SITA

BISHOPS ROAD

S.L.P 40326-00100 NAIROBI

SIMU: +254 -20- 2729800

KIPEPESI: +254-20- 2726497

BARUA PEPE : ps@labour.go.ke

TOVUTI : www.laboursp.go.ke